

# SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

[www.swahiliweb.net](http://www.swahiliweb.net)

Archive: Pat Caplan

Document: Mbibo Binti Hatibu

File reference: SW/PC/I3013

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Mbibo Binti Hatibu interviewed Kanga village 1985,  
transcribed 2010 Joseph Bwathondi**

*At the time of this interview, Mbibo was middle-aged and living alone, although she had adult children in the village. She was one of the wealthier women in Kanga, a situation she explained in terms of her hard work*

BH: Neno hilo kaweka Makungu Shirima. Nitamuua kama alivyomuua ng'ombe wangu, Halafu Makungu Shirima Yule Yule kaenda kwa Ali Manzi na kumueleza Ali Manzi "nimekuja kwako mwambie shangazi yako nitakapomuona pale nilipomfunga n'gombe wangu nitamuua kama alivyomuua n'gombe wangu na wale wanaofata fata nawauwa". Sasa neno lile kishaweka ripoti kwa mjumbe ameshaweka ripoti kwa mwanangu au sio, halafu ukachukue n'gombe kwako uje uwaweke kwenye shamba langu ndio maana gani?.

SK: Anataka ugomvi

BH: Aha! Ebu niambie Kiswahili kipo huku katika kichwa. Mimi kaniripoti kwa mjumbe. Mjumbe nakujulisha watu wako nitakapowaona kuchezea n'gombe wangu nitawafanya ninavyotaka. Unasikia?

SK: Ndio

BH: Sema moja

SK: Moja

BH: La pili bwana Baduru nimekuja kwako mwambie shangazi yako n'gombe wangu aliyekufa tarehe Fulani kamuuwa yeye. Na n'gombe wangu hasiwashike na akiwakaribia n'gombe wangu nilipowafunga, nitamfanya ninavyotaka. Sasa kaniambia nisiwakaribie n'gombe wake, nisiwashike, ehe! Na atanifanya anavyotaka leo kawachukua n'gombe toka nyumbani kwake na kuwatia shambani kwangu, kweli nitakosa mie kuingia shambani kwangu hata kutembea ndani ya shamba langu?

SK : Utaingia

BH: Ndio kuona vile nikaona Mungu akili yangu sina akili yoyote nikasema ngoja nikawaite watu wa serikali waje waone. Tendo lile alilonifanyia Makungu limeshafika. N'gombe nisiwashike, na ameshawafunga porini mwangu, n'gombe nimewauwa au sio?

SK: Mh!

BH: Kwake sasa kawaleta shambani kwangu kwa minajili gani? Kwake nilienda kuwauwa, sasa kuwaleta shambani kwangu kwa minajili gani? Niwamalize?

SK: Wamalize

BH: Sasa ndimi mie roho imenitoka nikaenda serikalini kuchukua baraza zima inihukumu mimi au Makungu. Nijue sasa mimi naambiwa makosi, akili ilinitoka sina heri imebadilika akili yangu sina. imebadilika kabisaa sina akili hata moja. Neno lile limetoka kwa mjumbe wa mtaa. Nitafanywa tendo kubwa. Neno lile liliwekwa kwa mtoto kuuwa, halafu n'gombe walele aniletee shambani mwangu awafunge? Je yeye akifa si itakuwa zaidi uchawi wangu? Sina maneno zaidi naishia hapa nakwenda kwa heri.

PC: Sasa amekusitaki wewe?

BH: Nimeenda kumshitaki mimi, jamani eeh kuna n'gombe shambani mwangu. Yule bwana kasema nisikanyage kwake naye kwangu sasa iweje leo anawaleta n'gombe wake shambani kwangu. Yeye alishaniambia mama kwangu husije. Sasa amekuja si kutafuta ugomvi

PC: Ndio

BH: Basi ndivyo ilivyokuwa ugomvi

PC: Sasa pesa za mpunga alilipa

BH: Pesa za mpunga ulee hakulipa, na akazaidi kuongeza maneno hayo simlipi mpunga na ngombe kawaleta shambani. Sasa hao shambani kawaleta nani? Simlipi bibi huyu pesa za mpunga kwa minajili n'gombe anafunga shambani mwake. Sasa huyu aliyewafunga ng'ombe shambani mwangu ni nani?? Na alishaniwekea ripoti bwana huyu? Kaweka ripoti kazungumza sana na kichwa kina faya kazi sawasawa kaniambia binti Hatibu hana ruhusa n'gombe wangu kuwakaribia lakini nipite kule maana nitawapulizia mie n'gombe wake watakufa. Unasikia akili yake ilivyompa. Nikishika kamba nimepulizia uchawi na n'gombe wake atakufa. Sasa kawachukua kwake kuwaleta shambani kwangu kusudio lake si kuja kuniua mara moja? Kaja siku hizi n'gombe magonjwa tele kaja kufia shambani mwangu halaa si atasema nimemuua. Tazama kwake kaniambia nimeenda je kawaleta

SH: Utawauwa

PC: Sasa utafanyaje

BH: Kufanyaji kwangu mimi nimekwenda mpaka wilayani mote kuweka ripoti hata na wewe ndugu(Pat) naweka ripoti huyu bwana anataka kuniuwa. Yeye mimi nae hatusemi, yeye kwake mie kwangu. Atawachukuaje n'gombe kuja kuwafunga shambani kwangu. Eh mama

PC: Sijuhi

BH: Sasa kashawafunga shambani kwangu na wekufa sasa kosa litakuwa juu ya nani si mimi nimewauwa?

PC: Kweli

BH: Sasa ule uchawi wangu si utazidi. Siku nyingine anaweza kuja kutia kitu kibaya shambani mwangu sababu nimpate Fulani nitamuwaje , unasemaje bwana Mgaza, hayo sawa tu. Sasa ndio mimi nikatoka kwenda kwa watu wa serikali na kwa kusema n'gombe , n'gombe sifaulu leo sio siku ya baraza itabidi kesho naweza enda nisiwape. Sasa nimekuja wazee mutazame manake mien a Makungu hatusemi. Na keshaniwekea ripoti kwa wakubwa sasa mie kwangu kaniwekeaje wanyama? Na wanyama wale nilikwishwa kuwauwa mimi? Na huyu mwanagu ndio kaja leo asubuhi ndio ninazungumza nae alhadullilah kama roho yangu ingekuwa nyeupe kama juzi na jana ningempa wasia wakizani.

PC: Haya

BH: Utakuja siku nyingine nitakuja kukupa na usia wa kizamani

PC: Haya mama

BH: ustarehe kidogo mama

PC: Haya mama

BH: Na mimi utanipa ya hidaya

PC: Hewala mama

BH: Na machungwa haya hapa ukale

PC: Haya mama

BH: Ukija tena kuna machungwa utaweza kununua hata gunia moja

PC: Gunia moja??

BH: Ukale tu mwangu.

AS: Na mume ndio huyu hapa ebu mpige nae picha

PC: Hataki anaogopa